

## 07-Adabu Za Kusoma Qur-aan

Kusoma Qur-aan ni 'ibaadah mionganoni mwa 'ibaadah anazokusudiwa Allaah (سبحانه وتعالى) Pekee; hivyo basi *maqurraa-a* wa Qur-aan wamependekeza mambo au mapambo ambayo yanapendeza ajipambe nayo kila anaetaka kusoma Qur-aan. Mionganoni mwa yaliyopendekezwa ni:

1. Kuweka udhu, kwa sababu Qur-aan ni mionganoni mwa *dhikru-Allaah* iliyo bora kabisa, japokuwa kisomo cha Qur-aan cha asiyekuwa na udhu kinajuzu.
2. Usafi na *twahaarah* ya nguo na mahali anapokaa kusoma kulingana na utukufu wa Qur-aan.
3. Kuelekea *Qiblah*.
4. Kuanza kwa *Isti'aadhah* na ma'ulamaa wengine wamewajibisha hili.
5. Kutoiacha *BismiLLaahi* mwanzo wa kila Suwrah isipokuwa *Suratut-Tawbah*.
6. Kuambatanisha *Isti'aadhah* na *BismiLLaahi* pale unapoanza Aayah zenyeye Majina ya Allaah (سبحانه وتعالى) na kutosoma *BismiLLaah* pale unapoanza na Aayah zenyeye kumtaja shaytwaan kuchunga kutoharibika kwa maana.
7. Kusoma kwa kutafakari na kuzingatia unachokisoma kama kwamba maneno ya Qur-aan unasemezwaa wewe kwani hili ndio kusudio na lengo kuu la kusoma Qur-aan; nako ni kufanya juu chini kuhakikisha kuwa moyo wako unashughulika na kuzingatia maana ya ukisomacho.
8. Kuisoma kwa utulivu, khushuu (unyenyekevu) wa kukhofu na kuheshimu maneno ya Mola Muumba, ambayo kama Anavyosema Mwenyewe (سبحانه وتعالى)

لَوْ أَنْزَلْنَا هَذَا الْقُرْءَانَ عَلَى جَبَلٍ لَّرَأَيْتَهُ خَشِعاً مُّتَصَدِّعًا مِّنْ خَشْبَةِ اللَّهِ<sup>ع</sup>

((Lau Tungeliiteremsha hii Qur-aan juu ya jabali, ungeliliona linanyenyekoa (na) lenye kupasukapasuka kutokana na khofu ya Allaah.))<sup>1</sup>

9. Kuisoma kwa *tartiyil*: Kuipa kila herufi haki zake inazostahiki kama kilivyokuwa kisomo cha Mtume (صلى الله عليه وسلم) na kama ilivyothibiti katika Hadiyth ya Anas bin Maalik (رضي الله عنه) alipoulizwa kuhusiana na kisomo cha Mtume (صلى الله عليه وسلم) alijibu kwa kusema: **"Kisomo chake kilikuwa cha kuvuta, kisha akasoma: BismiLLaahir-Rahmaanir-Rahiym: Akirefusha 'Allaah', na kurefusha 'Ar-Rahmaan', na kurefusha 'Ar-Rahiym"**<sup>2</sup>. Kupendezesha sauti yako kwani sauti nzuri ina athari zake katika nafsi ya msomaji mwenyewe na msikilizaji.
10. Kuathiriwa na Qur-aan, kwa kuomba kinga ya moto na adhabu, au kuomba maghfirah, Rehma, *Jannah* n.k. kila unapopitia Aayah zinazotaja hayo.
11. Kuathiriwa na Qur-aan , kwa kuhuzunika na kulia kwa kuguswa na maneno ya Allaah (سبحانه وتعالى). Kulia kwenye Aayah zenyе kutaja adhabu, kwa kujifikiria ulichokiacha au *kukiqassir* (kukipunguza).
12. Kutokukatiza kusoma kwa ajili ya kuzungumza na watu au kuitikia salaam ila ikihitajika.
13. Kusujudu katika Aayah zenyе alama ya *sijdah*.
14. Kunyanya sauti pale inapokuwa kuinyanya ni bora isipokuwa ikiwa utakhofia *riyaa-a* (kujionyesha), au kuwashawishi wenyе kuswali, basi kusoma kwa sauti ya chini wakati huu itakuwa bora kabisa.

---

<sup>1</sup>Al-Hashr (59: 21)

<sup>2</sup>Al-Bukhaariy